# HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA

## MUHTASARI WA MKUTANO WA BARAZA LA WAHESHIMIWA MADIWANI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA, ULIOFANYIKA TAREHE 28/10/2021

**KUMB.NA.CDC/BM/14/2021 WALIOHUDHURIA**

**A. WAJUMBE WALIOHUDHURIA**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mh. Bosco S. Mwanginde | Diwani Kata ya Mbugani | M/Kiti - H/W |
| 2. | Mh. Ramadhan A. Shumbi | Diwani Kata ya Mamba | M/M/Kiti - H/W |
| 3. | Mh. Christopher N. Mchaphu | Diwani Kata ya Kambikatoto | Mjumbe |
| 4. | Mh. Tusalimu S. Mwaijande | Diwani Kata ya Lualaje | Mjumbe |
| 5. | Mh. Mbwiga M. Mwasongole | Diwani Kata ya Mkola | Mjumbe |
| 6. | Mh. Junjulu N. Mhewa | Diwani Kata ya Sangambi | Mjumbe |
| 7. | Mh. Kasimu Y. Haule | Diwani Kata ya Makongolosi | Mjumbe |
| 8. | Mh. Rehema K. Mwamakula | Diwani Viti Maalum | Mjumbe |
| 9. | Mh. Sophia S. Mwanauta | Diwani Viti Maalum | Mjumbe |
| 10. | Mh. Geofrey Z. Kamaka | Diwani Kata ya Mafyeko | Mjumbe |
| 11. | Mh. Mkondo F. Malambughi | Diwani Kata ya Matwiga | Mjumbe |
| 12. | Mh. Nickson E. Mwankuga | Diwani Kata ya Mtanila | Mjumbe |
| 13. | Mh. Daniel G. Mwafyela | Diwani Kata ya Lupa | Mjumbe |
| 14. | Mh. Aden R. Tajack | Diwani Kata ya Nkung'ungu | Mjumbe |
| 15. | Mh. Richard N. Itelekelo | Diwani Kata ya Upendo | Mjumbe |
| 16. | Mh. Sailon M. Pashila | Diwani Kata ya Bwawani | Mjumbe |
| 17. | Mh. Kimo J. Choga | Diwani Kata ya Matundasi | Mjumbe |
| 18. | Mh. Samwel R. Komba | Diwani Kata ya Chokaa | Mjumbe |
| 19. | Mh. Alex J. Kinyamagoha | Diwani Kata ya Itewe | Mjumbe |
| 20. | Mh. Benson B. Msomba | Diwani Kata ya Kasanga | Mjumbe |
| 21. | Mh. Weston S. Mpyila | Diwani Kata ya Ifumbo | Mjumbe |
| 22. | Mh. Haji E. Chapa | Diwani Kata ya Chalangwa | Mjumbe |
| 23. | Mh. Mboka A. Konzo | Diwani Viti Maalum | Mjumbe |
| 24. | Mh. Phide K. Mwalukasa | Diwani Viti Maalum | Mjumbe |
| 25. | Mh. Neema N. Mwakaniemba | Diwani Viti Maalum | Mjumbe |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 26. | Mh. Sara D. Mwakilema | Diwani Viti Maalum | Mjumbe |
| 27. | Mh. Lenah H. Mboya | Diwani Viti Maalum | Mjumbe |

**B: WAJUMBE WASIOHUDHURIA**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mh. Masache N. Kasaka | - Mbunge | Kwa taarifa |
| 2. | Mh. Maryprisca W. Mahundi | - Mbunge Viti Maalum | Kwa taarifa |

**C: WATAALAMU**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Bibi. Esther H. Mwakalile | Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W) | Katibu |
| 2. | Bw. John F. Maholani | Afisa Utumishi na Utawala (W) | |
| 3. | Bibi. Janeth C. Mwaigoga | Kaimu Afisa Mipango (W) | |
| 4. | Bibi. Tabitha Haule | Kaimu Mweka Hazina (W) | |
| 5. | Bw. Cuthbert G. Mwinuka | Afisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika(W) | |
| 6. | Dr. Benedict N. Matogo | Afisa Mifugo na Uvuvi (W) | |
| 7. | Bi. Simphorose Kavishe | Kaimu Afisa Maliasili na Utalii (W) | |
| 8. | Bibi. Regina Ijiko | Kaimu Afisa Maendeleo ya Jamii (W) | |
| 9. | Bw. Joseph Halinga | Kaimu Mhandisi wa Ujenzi (W) | |
| 10. | Bw. Juma C. Mwajombe | Afisa Elimu Msingi (W) | |
| 11. | Bw. Hebel G. Kibona | Afisa Elimu Sekondari (W) | |
| 12. | Dr. John Gungumka | Kaimu Mganga Mkuu (W) | |
| 13. | Bw. Yohana L. Ngulukia | Afisa Mazingira na Udhibiti wa Taka Ngumu(W) | |
| 14. | Bw. Linus J. Mwanitega | Afisa Mtendaji Mkuu Mamlaka - M/M | |
| 15. | Bw. Eliya Benard | Mhasibu Mamlaka - M/M | |
| 16. | Bw. Godfrey A. Mwakibinga | Afisa Mipango Mamlaka - M/M | |
| 17. | Bibi. Salome P. Lyimo | Afisa Ugavi na Manunuzi (W) | |
| 18. | Bw. Hubert G. Matungwa | Mkaguzi wa Ndani (W) | |
| 19. | Bw. Alex S. Batwel | Afisa Uchaguzi (W) | |
| 20. | Bw. Happygod Mollel | Kaimu Afisa TEHAMA (W) | |
| 21. | Bw. James Sunge | Afisa Dawati la Malalamiko | |
| 22. | Bw. Arton J. Kayombo | Mthibiti Ubora Shule za Msingi na Sekondari(W) | |
| 23. | Adv. Athuman M. Bamba | Mwanasheria wa Halmashauri (W) | |
| 24. | Bi. Rehema Mwabulambo | Kaimu Afisa Nyuki (W) | |
| 25. | Bibi. Tabu T. Gavu | Mchumi | |
| 26. | Bw. Simon P. Mbela | Afisa Utumishi | |

| | | |
|---|---|---|
| 27. | Bw. Nerbert T. Gavu | Mchumi |
| 28. | Bw. Sunday Mwakalebela | Afisa Ardhi |
| 29. | Bw. Lodrick Y. Mwakisole | Afisa Biashara |
| 30. | Bw. Erick Nyoni | Afisa Tarafa Kiwanja |
| 31. | Bw. Kassim S. Kirondomara | Afisa Tarafa Kipembawe |
| 32. | Bw. Michael M. Msuya | Afisa Usafirishaji |
| 33. | Bw. Hope H. Musa | Afisa Utamaduni |
| 34. | Bw. Florian Mangasini | Afisa Mapato |
| 35. | Bw. Moses Ngole | Afisa Utumishi |
| 36. | Bw. David F. Ngowo | Mratibu TASAF |
| 37. | Bw. Mwayi S. Magomba | Afisa Ushirika |

**D: SEKRETARIETI**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Bibi. Simbabile O. Mbonile | Mwandishi wa Vikao |
| 2. | Bw. Robert L. Mfugale | Mwandishi wa Vikao |
| 3. | Bibi. Lucy D. Leza | Mwangalizi wa Ofisi |
| 4. | Bibi. Rehema A. Killah | Msaidizi wa Ofisi |

**E: WAALIKWA**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | WO.2 Mayeka S. Mayeka | Mkuu wa wilaya |
| 2. | Bw. anakleth Michombero | Katibu Tawala (W) |
| 3. | Desdelius Milanzi | Afisa Usalama wa Taifa (W) |
| 4. | SGT. Albert Jackson | Ag. MJAW |
| 5. | SGT. Osward C. Mwangosi | Ag. DFO |
| 6. | ASIS. Venance V. Luwagila | DIO |
| 7. | Sp. Amos A. Maheri | DPO |
| 8. | A/INSP. Elifazi R. William | Ag. OCD |
| 9. | Bw. Lutufyo Mwambungu | Kamanda PCCB (W) |
| 10. | Eng. Mang'ara M. Matiku | Meneja TARURA (W) |
| 11. | Eng. Lucas Mtabilwa | Meneja TANESCO |
| 12. | Bw. Yohana Mpamba | Kny. M/kiti CHADEMA |
| 13. | Bw. George Wayanga | Katibu CHADEMA |
| 14. | Bibi. Elizabeth Mwakatobe | Mjasiliamali |

15. Bw. Yakobo A. Mvanga    Mjasiliamali

**KUMB.NA.CDC/BM/15/2021 WIMBO WA TAIFA**

Mara baada ya viongozi na wajumbe kuingia ukumbini, wimbo wa Taifa uliimbwa.

**KUMB.NA.CDC/BM/16/2021 DUA YA KUIOMBEA HALMASHAURI**

Kabla ya kufungua mkutano, Mheshimiwa Mwenyekiti aliwaongoza wajumbe, wataalamu, wakaribishwa na waandishi wa habari kusoma dua ya kuiombea Halmashauri.

**KUMB.NA.CDC/BM/17/2021 KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti aliwashukuru Wajumbe na Wataalamu kwa mahudhurio yao. Akawakaribisha katika mkutano, akawajulisha wajumbe kuwa, tumeita baadhi ya Taasisi za Umma ili kupata ufafanuzi juu ya mambo mbalimbali yahusuyo Taasisi zao kama TARURA, RUWASSA na TANESCO. Akawataka kuwa makini katika kujadili agenda ya mkutano zilizokuwa mbele yao. Kisha akafungua mkutano saa 5:37 asubuhi.

**KUMB.CDC /BM/18/2021 KUTHIBITISHA AGENDA**

Katibu aliwasilisha agenda za kikao kama zinavyoonekana hapa chini;-

1. Wimbo wa Taifa
2. Dua ya Kuiombea Halmashauri
3. Kufungua Mkutano
4. Kuthibitisha Agenda za Mkutano
5. Maswali ya Papo kwa Papo
6. Kusoma na Kuthibitisha Muhtasari wa Tarehe 30/07/2021
7. Taarifa za Kamati za Kudumu
    - Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango
    - Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira
    - Kamati ya Elimu, Afya na Maji
    - Kamati Shirikishi ya Kudhibiti UKIMWI
    - Kamati ya Maadili ya Madiwani

8. Taarifa ya Utekelezaji wa Kazi za Matengenezo ya Barabara na Madaraja kwa Kipindi cha Julai, 2021 hadi Oktoba, 2021
9. Taarifa ya Kitengo cha Ardhi
10. Taarifa ya TANESCO
11. Salaamu toka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa
12. Mada ya Ujasiriamali
13. Mada ya ulinzi na usalama
14. Mada toka TAKUKURU
15. Mada toka Ofisi ya AMREF
16. Salaamu toka Chama Tawala
17. Taarifa ya Mafunzo ya Mgambo
18. Kufunga Mkutano

Mwenyekiti aliwaongoza wajumbe kuthibitisha agenda, wajumbe walikubali kuwa, zijadiliwe.

**KUMB.CDC /BM/19/2021 MASWALI YA PAPO KWA PAPO**
**Mh. Benson B. Msomba – Diwani wa Kata ya Kasanga**

**Swali na. 1.**
**(a)** Mh. Mwenyekiti kumekuwako na changamoto ya mahala pa kulala wale ndugu za wagonjwa (wanaouguza ndugu zao) kwa kipindi chote wanapokuwa hospitalini kuuguza, hali inayopelekea kutumia gharama kubwa kulala nyumba za wageni. Je, ni lini Halmashauri itakuwa tayari kujenga mradi wa hosteli ili kuwa accommodate watu hawa, na ukizingatia kuwa itachangia Halmashauri kujiongezea / kujipatia mapato, kwa vile watu hawa watakuwa wakilipia kiasi kidogo ili kujihifadhi hapo.

**Majibu:** Kwa utaratibu wa miundombinu ya Hospitali, Serikali inajenga majengo kwa ajili ya wagonjwa, siyo wauguzaji.

**(b)** Hospitali yetu ya wilaya kuna changamoto ya miundombinu ya kusafirishia maiti kutoka wodini kwenda mortuary pindi ikitokea mgonjwa amefia wodini, hali inayopelekea wauguzi kulazimika kubeba maiti mzega

mzega kupeleka mortuary. Je, Halmashauri imejipangaje kujenga miundombinu itakayowezesha vitololi vya kubebea maiti kutumika ili kuwarahisishia wauguzi kubeba maiti kwa kutumia vitendea kazi hivi ambavyo tunavyo.

**Majibu:** Katika mpango wa kuboresha miundombinu ya Hospitali, jengo la mortuary litaunganishwa kwa walk way na pia tutanunua kitanda cha kubeba wagonjwa mahututi na miili ya watu waliofariki kutoka wodini kwenda kwenye jengo la kuhifadhia maiti.

**Mh. Kimo J. Choga - Diwani wa Kata ya Matundasi**
**Swali na. 1.**
Je, Halmashauri haioni haja ya kuanzisha mradi wa biashara kwa maeneo ya baadhi ya shule za msingi na sekondari kwa kujenga frem za maduka ya kupangisha?

**Jibu:** Jambo hilo halitawezekana kwa sababu kwa kufanya hivyo tutakuwa tumechangia kuwaweka watoto (wanafunzi wa kike) katika mazingira magumu.

**Mh. Weston S. Mpyila - Diwani wa Kata ya Ifumbo**

**Swali Na. 1**
Mh. Mwenyekiti mikopo ya vikundi vya Vijana, Wanawake na Walemavu, imekuwa ikitolewa kwa muda sasa kutokana na maagizo ya Wizara (Serikali) vikundi vingi vimekuwa vikipewa pesa kidogo tofauti na pesa wanayoomba. Je, ni vigezo gani vinavyotumiwa kutoa pesa pungufu na ile vikundi vimeomba?

Je, hatuoni kama tunawakwamisha kutekeleza miradi yao kama walivyoainisha kwenye andiko la kuomba mkopo?

**MAJIBU:**

Vigezo vinavyotumiwa kutoa pesa pungufu tofauti na ilioyoombwa ni kama ifuatavyo;-

**1. Uhalisia wa Mradi Waliouandikia;**

Ni kwamba, ili kikundi kiweze kupatiwa mkopo ni lazima wataalamu wakitembelee kwa lengo la kuona uwepo wao, kuona uhalisia wa walichokiandikia, Idadi ya wanakikundi, gharama za vifaa walivyoandika, tunalinganisha gharama za uwekezaji na kipato tarajiwa.

**2. Ufinyu wa Bajeti;**

Mara nyingi maombi ya vikundi ni makubwa kuliko kiasi kilichotengwa, kwa hiyo inapotokea hali kama hivyo busara hutumika, badala ya kukikosesha kikundi kisipate fedha, tunaamua kupunguza kiasi ili wote waenee.

**3. Udanganyifu;**

Uzoefu umeonesha kuwa, baadhi ya vikundi siyo wakweli na watu hawana miradi ya pamoja. Kinachotokea pindi wanapopata fedha wanagawana na kupelekea ugumu wa marejesho.

**N.B.** Hata hivyo Halmashauri yetu ni miongoni mwa Halmashauri nchini zinazofanya vizuri katika utoaji wa mikopo.

**Mh. Alex J. Kinyamagoha - Diwani wa Kata ya Itewe**

**Swali na. 1.**

Kwa kuwa Chunya ipo katika mradi wa urejeshaji wa ikolojia na baianowai, ni lini Kamati ya Elimu, Afya na Maji itafanya ziara kutembelea bwawa la Nzingwa kujionea athari zilizopelekea Viboko kuhama na kutembelea bonde la mto Lupa na kuzungumza na kamati ya matumizi ya maji bonde la mto Lupa?

**Majibu:** Kuhusu Kamati ya Elimu, Afya na Maji kufanya ziara ya kutembelea bwawa la Nzingwa kujionea athari zilizopelekea Viboko kuhama na kutembelea bonde la mto Lupa na kuzungumza na kamati ya matumizi ya

maji bonde la mto Lupa haitawezekana kwa sababu fedha hazikutengwa kwenye bajeti ya Halmashauri.

**Swali na. 2**. Migogoro mingi ya ardhi kwa sasa ni ile ya wachimbaji na makundi mengine wakiwemo wakulima na wafugaji, na sehemu kubwa ya migogoro hii hutokana na sheria ya utoaji wa leseni za utafutaji na uchimbaji wa madini pamoja na mfumo wa uombaji na utoaji leseni za madini (mining cadasca portal), licha ya Serikali kuanzisha mpango wa matumizi bora ya ardhi, napenda kujua Je, Serikali ina mpango gani ili kubadilisha ama kurekebisha sheria hizi ambazo zinachochea uwepo wa migogoro hii?

Na kwa kuwa migogoro hii ni mingi hapa Chunya, Je, wilaya ina mpango gani kuanzisha baraza la ardhi la wilaya, kuwaondolea watu usumbufu wa kusafiri hadi Mbeya kupata haki ya usuluhishi wa migogoro hii?

**Majibu:** Kutokana na migogoro ya ardhi kuwa mingi, Serikali imeanzisha mchakato wa kuweka baraza la Ardhi katika Wilaya ya Chunya. Na tayari Mkurugenzi Mtendaji (W) na Mkuu wa Wilaya wanatafuta jengo ambapo Ofisi ya Baraza itaanzishwa. Pia Serikali imewateua vijana wanne (04) katika wilaya ya Chunya kujiunga na Baraza la Ardhi kwa barua maalum. Vijana hao ni;- Bi. Flora Mihayo na Bw. Lusekelo Kibona, hawa wanatokea Tarafa ya Kiwanja. Bw. Deusdedith M. Gombanila na Bibi Ashura A. Salim, hawa wanatokea Tarafa ya Kipembawe.

**KUMB.CDC /BM/20/2021 KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA MKUTANO WA BARAZA LA WAHESHIMIWA MADIWANI WA TAREHE 30/07/2021**

Muhtasari ulisomwa, wajumbe walikubali kuwa ulikuwa kumbukumbu sahihi, mwenyekiti aliusaini kuuthibitisha.

**KUMB.CDC /BM/21/2021 TAARIFA ZA KAMATI ZA KUDUMU**

**A: TAARIFA YA KAMATI YA FEDHA, UTAWALA NA MIPANGO**

Mheshimiwa Tusalimu S. Mwaijande, Diwani wa Kata ya Lualaje kwa niaba ya Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri, aliwasilisha taarifa ya Kamati ya

Fedha, Utawala na Mipango iliyohusu taarifa ya mapato na matumizi ya Halmashauri kwa kipindi cha mwezi Julai, 2021, taarifa ya makisio ya mapato kwa kila kata kwa mwaka, 2021/2022, taarifa ya mapato na matumizi ya Mamlaka ya Mji Mdogo Makongolosi kwa kipindi cha mwezi Julai, 2021, mpango wa manunuzi ya Halmashauri kwa mwaka wa fedha, 2021/2022,pendekezo la kuingia mikataba ya upangaji katika vibanda nane (08) katika soko la Uhindini na kituo cha mabasi Chunya Mjini na pendekezo la kuanzishwa kwa kata mpya tano (05) na vijiji vipya kumi(10).

Pia aliwasilisha taarifa ya mapato na matumizi ya Halmashauri kwa kipindi cha Julai hadi Agosti, 2021, taarifa ya mapato na matumizi ya Mamlaka ya Mji Mdogo Makongolosi kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Agosti, 2021, ombi la kibali cha ajira sita (06) za madereva kwa mkataba na mengineyo kuhusu wajumbe na wataalamu kushiriki kikamilifu katika mapokezi ya mbio za Mwenge wa Uhuru, 2021.

Vile vile aliwasilisha taarifa ya mapato na matumizi ya Halmashauri kwa kipindi cha Julai hadi Septemba, 2021, taarifa ya mapato ngazi ya kata kwa kipindi cha Julai hadi Septemba, 2021 (robo ya kwanza, 2021/2022), mabadiliko ya watia saini katika akaunti za Halmashauri, taarifa ya mapato na matumizi ya Mamlaka ya Mji Mdogo Makongolosi kwa kipindi cha Julai hadi Septemba, 2021, taarifa ya ujio wa wawekezaji kampuni ya uchimbaji ya Shanta, pendekezo la mabadiliko ya tozo za ukaguzi wa nyama na usafi wa machinjio, taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kipindi cha robo ya kwanza, 2021/2022 (Julai hadi Septemba, 2021) na taarifa ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo kwa kipindi cha robo ya kwanza, 2021/2022 (Julai hadi Septemba, 2021).

Mheshimiwa Tusalimu S. Mwaijande pia aliwasilisha taarifa ya kitengo cha manunuzi kwa kipindi cha robo ya kwanza, 2021/2022, taarifa ya Idara ya Utumishi na Utawala kwa kipindi cha robo ya kwanza, 2021/2022, taarifa ya Kitengo cha sheria kwa kipindi cha robo ya kwanza, 2021/2022, ombi la kuanza taratibu za upangishaji katika soko la madini na mengineyo.

Wajumbe walipokea na kujadili taarifa hiyo, aidha kuhusu upangishaji katika soko la madini wajumbe walisisitiza kuwa;-

- Wafanyabiashara waliopo katika soko la madini la sasa wapewe kipaumbele katika soko la madini la Halmashauri.

Kuhusu mafunzo kwa mabaraza ya kata, wajumbe walitaka kujua ni lini mabaraza hayo yatajengewa uwezo. Ufafanuzi ulitolewa kuwa, mafunzo yameshaanza kutolewa na yataendelea kutolwa kwa kata ambazo bado.

Vile vile wajumbe walitaka kujua kuhusu ushuru wa huduma unakusanywaje au kwa nini mchimbaji aliyeuza dhahabu asipewe risiti wakati ndiye aliyekatwa ushuru wa huduma wa asilimia 0.03. ufafanuzi ulitolewa kuwa, Halmashauri wanamkata mnunuzi na kumpa risiti. Halmashauri haitoi risiti kwa muuzaji.

**B: TAARIFA YA KAMATI YA UCHUMI, UJENZI NA MAZINGIRA**

Mheshimiwa Christopher N. Mchaphu, Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira aliwasilisha taarifa ya kamati yake iliyohusu taarifa ya Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika kwa kipindi cha robo ya kwanza, 2021/2022, taarifa ya Idara ya Mifugo na Uvuvi kwa kipindi cha robo ya kwanza, 2021/2022, taarifa ya Idara ya Ardhi na Maliasili kwa kipindi cha robo ya kwanza, 2021/2022, taarifa ya Kitengo cha Nyuki kwa kipindi cha robo ya kwanza, 2021/2022, taarifa ya Idara ya Mazingira na Udhibiti wa Taka Ngumu kwa kipindi cha robo ya kwanza, 2021/2022 na mengineyo.

Wajumbe walipokea na kujadili taarifa hiyo, kisha walipitisha.

**C: TAARIFA YA KAMATI YA ELIMU, AFYA NA MAJI**

Mheshimiwa Tusalimu S. Mwaijande, Mwenyekiti wa Kamati ya Elimu, Afya na Maji aliwasilisha taarifa ya kamati yake iliyohusu taarifa ya Idara ya Elimu Msingi kwa kipindi cha robo ya kwanza, 2021/2022, taarifa ya Idara ya Elimu Sekondari kwa kipindi cha robo ya kwanza, 2021/2022, taarifa ya Idara ya Afya kwa kipindi cha robo ya kwanza, 2021/2022 na mengineyo.

Wajumbe walipokea na kujadili taarifa hiyo, kisha waliipitisha.

**D: TAARIFA YA KAMATI SHIRIKISHI YA KUDHIBITI UKIMWI**

Mheshimiwa Benson B. Msomba, Diwani wa kata ya Kasanga kwa niaba ya Mheshimiwa Ramadahani A. Shumbi, aliwasilisha taarifa ya Kamati Shirikishi ya kudhibiti UKIMWI iliyohusu taarifa ya mapambano dhidi ya UKIMWI toka Idara ya Maendeleo ya Jamii kwa kipindi cha robo ya kwanza, 2021/2022, taarifa ya mapambano dhidi ya UKIMWI toka Idara ya Afya kwa kipindi cha robo ya kwanza, 2021/2022, taarifa za makundi mbalimbali yanayojihusisha na mapambano dhidi ya UKIMWI kama ADP – Mbozi, WAVIU, kundi la wazee na madhehebu ya Kidini (Dini ya Kikristo na Dini ya Kiislam)

Wajumbe walipokea na kujadili taarifa hiyo, kisha walipitisha.

**E: TAARIFA YA KAMATI YA MAADILI**

Mheshimiwa Mbwiga M. Mwasongole, Diwani wa Kata ya Mkola aliwasilisha taarifa ya kamati yake ambapo katika taarifa hiyo ilisisitizwa Wajumbe (Waheshimiwa Madiwani ) kushiriki kwenye shughuli/matukio ya Kitaifa kama mapokezi ya Mbio za Mwenge wa Uhuru.

Wajumbe walipokea na kujadili taarifa hiyo, kisha waliipitisha.

**KUMB.CDC /BM/22/2021 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA KAZI ZA MATENGENEZO YA BARABARA NA MADARAJA KWA KIPINDI CHA JULAI HADI OKTOBA, 2021.**

Meneja wa TARURA (W) aliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa kazi za matengenezo ya barabara na madaraja kwa kipindi cha Julai hadi Oktoba, 2021 ambapo aliwajulisha wajumbe kuwa, wilaya ya Chunya ina mtandao wa barabara wenye jumla ya KM. 840.1 zilizogawanyika kiutawala. KM. 260.8 zinasimamiwa na Meneja wa TANROAD Mkoa. Hizi zinahusisha barabara kuu na za Mkoa.

Wajumbe walipokea na kujadili, kisha walishauri kuwa;-

- Wakandarasi wakifika katika maeneo ya kazi washauriane na Waheshimiwa Madiwani wa maeneo husika.
- Mtandao wa barabara uongezeke kulingana na mapendekezo yaliyowasilishwa Ofisi za TARURA (W).
- Barabara ya Makongolosi hadi Ujerumani makalvati yanayostahili.

Kuhusu barabara ya Sipa, wajumbe walitaka kujua ni lini itakamilika. Ufafanuzi ulitolewa kuwa, wakandarasi wapo katika hatua ya maandalizi ya mitambo, kisha watafika saiti.

Baada ya kujadili, wajumbe walishauri kuwa;-

- Wakandarasi wafike mapema kabla ya mvua kuanza, vinginevyo mvua zitakapochanganya, barabara hazitapitika.
- Katika matengenezo yote ya barabara, mifereji ipewe kipaumbele ili kuepuka uharibifu wa barabara usiokuwa wa lazima.

**KUMB.CDC /BM/23/2021 TAARIFA YA KITENGO CHA ARDHI**

Afisa Ardhi aliwasilisha mapendekezo ya michoro kumi na saba (17) ya mipango miji yenye viwanja 318 vyenye matumizi mbalimbali ili kukidhi mahitaji ya jamii, iliyoandaliwa katika kata kumi na moja (11) ambazo ni Sangambi, Mbugani, Chalangwa, Ifumbo, Kasanga, Matundasi, Bwawani, Makongolosi, Mkola, Itewe na Chokaa, Tarafa ya Kiwanja ambapo rasimu ya ramani zake/michoro yake imeoneshwa hapa chini;-

(Michoro na. 06/CHY/01/062021, 06/CHY/02/062021, 06/CHY/03/062021, 06/CHY/04/062021, 06/CHY/05/062021, 06/CHY/06/062021, 06/CHY/07/062021, 06/CHY/08/062021, 06/CHY/09/062021, 06/CHY/10/062021, 06/CHY/11/062021, 06/CHY/12/062021, 06/CHY/13/062021, 06/CHY/14/062021 na 06/CHY/15/062021, 06/CHY/16/062021, 06/CHY/17/062021.

Pia inapendekezwa ramani ya kata ya Mbugani iwe ya mfano katika wilaya ya Chunya kwa kupanga nyumba zenye hadhi na zenye rangi moja katika kitalu kimoja kimoja. Mfano; Block na. 1, bati ziwe za rangi ya kijani, Block na. 2, bati ziwe za rangi ya bluu, Block na. 3, bati ziwe za rangi ya karoti.

Aidha inashauriwa barabara zifunguliwe kabla ya mvua kunyesha ili kuuboresha mji wetu wa Chunya.

Wajumbe walipokea na kujadili mapendekezo hayo. Aidha walitaka kujua kama Kitengo cha Ardhi kimeanza mchakato wa kuvifanya vijiji kuwa mitaa katika mji wa Chunya. Ufafanuzi ulitolewa kuwa, mchakato umeshafanyika. Pindi utakapokamilika, vijiji vitabadilishwa kuwa mitaa.

Vile vile wajumbe walitaka kujua kama mpango huo unahusisha Tarafa ya Kipembawe au hauhusishi. Ufafanuzi ulitolewa kuwa, mpango huu ni endelevu. Utakapofika muda wa upimaji kwa Tarafa ya Kipembawe, vijiji vyote vya Tarafa ya Kipembawe vitapimwa.

Baada ya kujadili taarifa hiyo iliyohusu mapendekezo ya michoro kumi na saba (17) ya mipango miji yenye viwanja 318 vyenye matumizi mbalimbali, wajumbe walipitisha.

**KUMB.CDC /BM/24/2021 TAARIFA YA IDARA YA MAJI (RUWASA)**

Meneja wa RUWASA (W) aliwasilisha taarifa iliyohusu miradi iliyotekelezwa na inayoendelea kutekelezwa ikiwa ni pamoja na ukamilishaji ujenzi wa Bwawa la maji la Matwiga, mradi wa maji Makongolosi, mradi wa maji Matundasi, mradi wa maji Sangambi, Ifumbo kwa ufadhili wa UNICEF, Mlimanjiwa, Kambikatoto, Kasanga, Chalangwa, Mkola na Mapogoro.

Wajumbe walipokea na kujadili, aidha walitaka kujua kama mgogoro wa sambazaji mabomba ya maji umetatuliwa kutokana na wananchi walio wengi kutofikiwa. Ufafanuzi ulitolewa kuwa, mradi huo mpya haujakamilika kwa asilimia 100. Shughuli za ufungaji wa mabomba unaendelea. Jumla ya Kilomita 7 zimeongezwa ili kuwafikia wananchi kwa idadi kubwa.

Hata hivyo wajumbe walitaka kujua, lini kisima cha maji kilichochimbwa Sangambi kitaanza kutoa maji. Ufafanuzi ulitolewa kuwa, kisima hicho kitaanza kutoa maji mara kitakapokamilika.

Baada ya kujadili, wajumbe walishauri kuwa;-

- Mamlaka ya Maji Chunya Mjini ikae na wateja wake wa maji ili wasikilize kero zao na kuzipatia ufumbuzi.

**KUMB.CDC /BM/25/2021 TAARIFA YA SHIRIKA LA UMEME TANZANIA (TANESCO)**

Meneja wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) wilaya ya Chunya, aliwasilisha taarifa toka kwenye shirika lake iliyohusu hali ya umeme, idadi ya wateja, wateja wakubwa, uunganishaji wa wateja wapya, changamoto na mikakati ya kukabiliana na changamoto hizo.

Wajumbe walipokea na kujadili taarifa hiyo. Aidha walitaka kujua ni lini changamoto ya umeme itatatuliwa katika kijiji cha Itumbi. Ufafanuzi ulitolewa kuwa, hadi ifikapo tarehe 30/12/2021, uunganishaji umeme katika kijiji cha Itumbi utakuwa umeshaanza.

Baada ya kujadili taarifa hiyo, wajumbe walipitisha.

**KUMB.CDC /BM/26/2021 SALAAMU ZA MKOA**

Mwakilishi wa Katibu Tawala Mkoa aliwasilisha salaamu za Mkoa ambapo alianza kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa fedha nyingi za utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Wilaya ya Chunya. Akawapongeza pia viongozi na wataalamu wa Halmashauri ya wilaya ya Chunya kwa kazi nzuri za usimamizi na utekelezaji wa miradi ya maendeleo na makusanyo ya mapato ya ndani na udhibiti wa mapato ya ndani. Aidha akasisitiza kuongeza kasi ya ukusanyaji wa mapato fungwa.

Hata hivyo akaagiza kuwa;-

- Fedha kiasi cha Tsh. 300,000,000/= zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya cha Mafyeko, zihamishe na kupelekwa katika Kituo cha Afya cha Isangawana ili kukamilisha ujenzi. Aidha Waheshimiwa Madiwani wasimamie utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kuzingatia fedha zilizotolewa na Mheshimiwa Rais kwa kata zote.

**KUMB.CDC /BM/27/2021 MADA YA UJASILIAMALI**

Mheshimiwa Mwenyekiti alimkaribisha mjasiliamali Bibi. Elizabeth Mwakatobe wa Mbeya kuwasilisha mada yake ya ujasiliamali. Bibi. Elizabeth aliwasilisha mada yake ikiwa ni pamoja na kuwaonesha wajumbe baadhi ya kazi zake za mikono kama ufumaji wa masweta na skafu. Akawasilisha ombi lake la kufanya kazi na Halmashauri ya wilaya ya Chunya kwa kusambaza bidhaa zake kwenye shule za msingi na sekondari. Aidha yuko tayari yuko tayari kulipa kodi kwa ajili ya kuchangia maendeleo ya Halamshauri ya wilaya ya Chunya.

**KUMB.CDC /BM/28/2021 SALAAMU ZA MKUU WA WILAYA**

Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Chunya alianza kwa kumshukuru Mheshimiwa Mwenyekiti wa Halmashauri kwa kumpa nafasi ili awasilishe salaamu za Ofisi yake. Aidha alimshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa fedha kiasi cha Tsh. Bilioni 4.6 utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Wilaya ya Chunya.

Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya pia alizungumzia kuhusu upotevu wa vifaa vya ujenzi katika Kituo cha Afya cha Makongolosi ambapo alimwagiza Mkurugenzi Mtendaji (W) yafuatayo;-

- Watuhumiwa wote wafikishwe mahakamani.
- Iundwe tume ya watu wachache ifanye uchunguzi ili kujua ukweli na upana wa changamoto ya upotevu wa vifaa vya ujenzi katika Kituo cha Afya cha Makongolosi
- Watakaobainika kuhusika na upotevu wa vifaa vya ujenzi katika Kituo cha Afya cha Makongolosi wawajibishwe kisheria.

Vile vile alizungumzia kuhusu ukamilishaji ujenzi wa soko la madini, hospitali ya wilaya, utendaji usioridhisha wa wataalamu wa TARURA, malalamiko ya wafanyabiashara wa mkaa kuhusu tozo za mkaa, uuzaji wa viwanja, uanzishwaji radio ya Halmashauri, usafi wa mazingira na fedha Tsh. 300,000,000/= za ujenzi wa Kituo cha Afya cha Mafyeko, alisisitiza kuwa;-

- Fedha hizo zipelekwe katika Kituo cha Afya cha Isangawana ili kukamilisha ujenzi badala ya kuanzisha ujenzi mpya.
- Fedha za ujezi wa shule ya sekondari Lualaje zipelekwe kujenga sekondari Lualaje kama ilivyopangwa awali badala ya Kambikatoto na kazi ianze mara moja.
- Wakati wa kupangisha vyumba kwenye soko la madini la Halmashauri, wafanyabiashara waliopo katika soko la sasa wapewe kipaumbele.
- Hospititali mpya ya wilaya ijengwe mahali ilipo Hospitali ya sasa, isipokuwa ushauri wanamna ya kuingiza majengo mapya utolewe na wataalamu.
- Halmashauri itoe fidia fedha kwa wamiliki wa viwanja ili kupata wiwanja vitakavyopimwa na kuuzwa.
- Meneja wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO ) afuatilie utendaji kazi wa wataalamu wake ili wala rushwa wawajibishwe.
- Halmashauri ione uwezekano wa kuanzisha radio.
- Waheshimiwa Madiwani wasaidie kuhamasisha kuhusu usafi wa mazingira katika maeneo yao.
- Ujenzi wa majengo mapya uzingatie ramani za mipango miji.

**Neno la shukrani:**

Mheshimiwa Tusalimu S. Mwaijande, kwa niaba ya Waheshimiwa Madiwani wote, alimshukuru Mheshimiwa Mkuu wa wilaya ya Chunya kwa hotuba yake na kuahidi kuyafanyia kazi maagizo na maoni yake.

**KUMB.CDC /BM/29/2021 MADA YA ULINZI NA USALAMA**

Mwakilishi wa Kamanda wa Jeshi la Polisi (W) aliwasilisha mada ya ulinzi na usalama ambapo aliainishaa maeneo hatarishi. Aidha alisisitiza kuimarisha ulinzi na usalama kwenye maeneo yao ya makazi kwa kuunda vikundi vya ulinzi shirikishi.

**KUMB.CDC /BM/30/2021 MADA TOKA TAKUKURU**

Kamanda wa TAKUKURU (W) aliwasilisha mada kuhusu mapambano dhidi ya rushwa ambapo alisisitiza yafuatayo;-

- Usimamizi wa fedha za miradi.
- Uvamizi wa maeneo ya hifadhi na -
- Watendaji wa Kata na Vjiji kuwatoza faini kubwa wananchi waliokosa

**KUMB.CDC /BM/31/2021 MADA YA USAFI WA MAZINGIRA TOKA AMREF**

Mwakilishi wa Shirika la MREF aliwasilisha mada ya usafi wa mazingira lengo likiwa ni kuboresha usafi wa mazingira kwenye shule za msingi, uboreshaji wa vyoo ambapo zaidi ya matundu 48 yanaendelea kujengwa kwa sasa, ujenzi wa maeneo ya kunawia mikono na ufundishaji wa mafundi juu ya ujenzi wa vyoo bora.

**KUMB.CDC /BM/32/2021 SALAAMU TOKA CHAMA TAWALA (C.C.M)**

Mwakilishi wa Katibu wa Chama cha Mapinduzi (C.C.M) Chama Tawala, Mheshimiwa Zaituni O. Sembo aliwasilisha salaamu za chama chake ambapo alianza kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa fedha nyingi za utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Wilaya ya Chunya. Akasisitiza kuendeleza mshikamano na ushirikiano katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kumuunga mkono Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**KUMB.CDC /BM/33/2021 SALAAMU TOKA OFISI YA MSHAURI WA KIJESHI**

Mshauri wa Kijeshi alianza kwa kumshukuru Mheshimiwa Mwenyekiti wa Halmashauri kwa kumpa nafasi. Aidha akawajulisha wajumbe kuwa, mafunzo ya jeshi la mgambo kwa Tarafa ya Kiwanja yamekamilika. Aidha kwa Tarafa ya Kipembawe yatafanyika mwaka 2022.

**KUMB.CDC /BM/~~13~~ 34/2021 KUFUNGA MKUTANO**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe, wataalamu, waalikwa na waandishi wa habari kwa kufanikisha Mkutano. Akasisitiza yafuatayo;-

- Waheshimiwa Madiwani wapeleke mrejesho wa Mkutano wa Baraza la Madiwani kwa wananchi.

- ❖ Waheshimiwa Madiwani wasimamie kwa karibu utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwenye maeneo yao.
- ❖ Waheshimiwa Madiwani wahamasishe wananchi kulipa kodi kwa hiari.

Akamalizia kwa kusisisitiza Wananchi kutunza chakula walichonacho na kulima mazao yanayokomaa kwa muda mfupi kwa kuwa huenda mvua zikawa chache kwa msimu wa mwaka 2021/2022. Hii ni kutokana utabiri wa Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini. Kisha akafunga mkutano saa 9:31 mchana.

**UMETHIBITISHWA**

……………………

**BW. TAMIM H. KAMBONA**
**KATIBU**

……………………

**MH. BOSCO S. MWANGINDE**
**MWENYEKITI**

28/01/2022
……………………
**TAREHE**